

Please prepare a good literary translation of the entire passage in the time allowed. Use of a dictionary is permitted. Choose one of the two passages.

passage: 1

TIME: 2 hours

TITLE: "Kazi za Kawaida: Wanyamwezi wajao pwani"

Baada pembe kupigwa chapa, siku ya kutaka biashara huenda yule Mnyamwezi mwenye pembe zake pamoja na rafiki yake hata dukani kwa Mhindi na watapangia pembe. Biashara yao pembe moja anataka vitu vya duka lote, lakini Wahindi mahodari wa biashara hizo. Wanaanza mwanzo wa asubuhi hata saa sita, wala pembe moja haijesha. Mara anataka rangi hii, mara anataka rangi hii. Na katika biashara yao, sharti waletewe tende na nazi, hufurahi sana, husema, Mhindi huyu mzuri sana, anajua kufanya biashara. Mhindi husema, Nnawapa bure, hapana hesabu katika uguzi wetu. Lakini yeye Mhindi huandika yote katika daftari yake.

Kisha watarejea maneno ya biashara, hata wagombane waka-sema, Sasa njaa zitama, leo tuache uguzi, kesho tutakuja. Siku ya pili watakwenda na kama hawakupatana haitakwisha biashara. Labda siku ya tatu Mhindi atapatana na yule Mswahili, Semana na rafiki yako, biashara iishe. Naye atampa maneno mazuri yule Mnyamwezi, atakata biashara. Na kukata kwake atawatukana wote wawili Mnyamwezi na yule Mhindi, huwaambia, Ninyi wajinga, hamjui biashara. Humwuliza Mnyamwezi, Unataka nini, na Mhindi nini hataki kukupa? Husema, Nataka rangi kadha wa kadha. Humwuliza yule Mhindi, Huna hasara? Hujibu, Ninayo hasara. Husema, Haidhuru, mpe kitu atakacho, sababu utanunua pembe nyingi kwake. Atampa. Baada yake haiishi biashara, ila wanyapara walio katika biashara wapate heshima yao kitambi au nguo nyingine. Atawashika mkono awapatanishe. Hii ndiyo biashara yao Wanyamwezi.

Baada ya biashara kwisha, Wanyamwezi huenda kokoni¹⁰ kukata mambo.¹¹ Mambo zao fito za kufungia mitumba. Kisha hupewa upagazi wao wa kurejea bara. Hununua vitu watakavyo.

Tena hufunga mitumba, mtumba mmoja ndani yake mna jora kumi na vitambi, na uchukuzi wao wanachukulia begani. Nao wanawake na wanaume huchukua mizigo. Na iwapo amenunua vitakataka vingi, naye lazima kuchukua mtumba wa watu, na vitu vyake hufunga kiunoni.]

KAZI NI MAENDELEO katika utamaduni wetu
 Kama ilivyodokezwa katika utangulizi, madhumuni
 ya kitabu hiki yamekuwa ni kusisitiza thamani ya
JEMBE NA UFUNDI kama vyombo muhimu katika
 utamaduni wetu. Jembe na ufundi vimechukuliwa kama
 vilelezo vya jumla ya mambo yote yanayofanya utama-
 duni wa Mtanzania. Vipengele muhimu vya Kilimo,
 Uchumi, na Siasa, Afya na Chakula Bora vimechaguliwa
 na kuhusishwa na Jembe na Ufundi wa jadi yetu toka
 kipindi cha ujima, ukoloni, uhuru na baada ya Azimio
 la Arusha ili kuonyesha kuwa Jembe na Ufundi vilikuwa,
 na bado vinaendelea kuwa muhimu sana kwa jamii yetu
 katika jitihada zake za kujidumisha na kujiendeleza.

UTAMADUNI NI KAZI

Katika kitabu hiki imesisitizwa kuwa utamaduni ni
 jumla ya mawazo, fikra na mambo yote yanayozingatwa
 na jamii katika mbinu zake za kujidumisha na kujiende-
 leza. Utamaduni ni kitu chochote ambacho mtu anakifanya
 katika mazingira yake. **UTAMADUNI NI KAZI.**

Historia ya taifa letu ni historia ya sifa na fahari
 kwa sababu wazee wetu walizingatia **KAZI**. Kutokana na
 maarifa na ufundi wao walioweza kutengeneza jembe na
 vifaa vingine na kuvitumia kwa kilimo kujipatia chakula
 na ruzuku zao nyingine za maisha. Kutokana na ufundi
 na uhodari wao walitengeneza silaha na kupambana
 kiume na wadhalimu wa kigeni katika vita vya Biashara
 ya Watumwa na vita vya Maji Maji. Kutokana na maarifa
 na ufundi wao waliweza kutengeneza vyombo vya nyu-
 mbani na sanaa. Baadhi ya vyombo hivyo vilitumiwa na
 wao wenyewe na vingine waliuza. Maarifa, ufundi na
 juhudi ziliwaletea wazee wetu sifa na fahari kubwa. Wazee

wetu walitambua barabara kuwa **KAZI** ndio msingi wa
 maisha, heshima ya binadamu na ustawi wa jamii nzima.

Tumepaswa kuyapokea mawazo na fikra hizo kama
 urithi wetu mkubwa. Ni lazima tujivunie utamaduni wetu
 kwani utamaduni ndio uti wa mgongo wa jamii au taifa
 lolote. Ni lazima tupende **KAZI**. Daima tuwe tayari
 kupambana na mazingira yetu kwa juhudi na maarifa.
 Uzururaji, uzembe na ulevi uwe kwetu mwiko. Twapaswa
 kutambua kuwa wajenzi wa taifa letu ni sisi wenyewe na
 tutalijenga tu taifa letu kwa kila mmoja wetu. **KUFANYA**
KAZI na kutimiza wajibu wake, tukiamini kuwa:

**KAZI NI UTU, KAZI NI MAENDELEO NA
 KAZI NI UHAI!**